

## Average Insha KCPE 2003

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu juu ya kichwa kifuatacho: HASIRA HASARA  
Siku yenyewe ilikuwa Ijumaa. Nakumbuka vizuri sana namna baba alivyoingia nyumbani ..... Endeleza.

akiwa mlevi. Nguo zake zilikuwa zimechafu  
Alikuwa na matope kutoka Kichwani hadi  
miguuni. Alipokuwa akivaa hizo nguo zilikuwa  
nyupe, pe pe pe na zikimetameta metu metu.  
Hungenjya rangi ya nguo kwa sababu ya  
matope mingi.

Mamangu alipomwona akiingia kwa  
mlango alijawa na hasira. Hakutaka kuzungum-  
saye. Yeye alimwekea chakula changi. Wakeni  
hawakuhosea waliponena hasira hasira. Babangu  
alimwambia mamangu ansafishie viatu. Mamangu  
hakutaka kuzisafisha. Babangu alijawa na  
hasira na akamtandika mamangu. Alimtandika  
karibu amue. Mama alikuwa tu akipiga mayow  
Dadangu na mimi tulijaribu kumpoleza. Lakini  
alianza kututandika na akatupeleka tukala  
Alitufunika gumbi gumbi na tukalala fo fo.

Siku iliyofuata ya Jumamosi nili-  
amka asubuhi na mapema. Ndege wali'kuwa  
wakiimba nyimbo zao kwa sauti nyoro. o  
kama ya kinanda kukaribisha siku. Nili  
jiesha uso na nikapiga mswaki. Nilimkuta  
mamangu jikoni akitayarisha kiamcha kin-  
wa. Hakuwa na furaha hata kidogo. Alir

uwa akilia kwa uchungu. Machozi yalimt ririka tiri tiri. Hata hakunisalimia kama kawaida.

Baada ya kiamcha - kinywa kuiva nili-peleka mezani. Babangu aliamka na okajio-go mwili. Alipomaliza kunywa alienda kazi ni. Baada ya babangu kuondoka mama alienda hospitali. Alitimbiwa na akaonekana kwamba alikuwa anefunjika mguu. Alitimbiwa mguu na akanudi nyumbani.

Siku hiyo baba alikuja kama kawaida. Hakuwa amelewa. Alipoangalia mama aliona anefunjika mguu. Alimwomba mama msamaha na akasema kutoka siku hiyo hatakunywa pombe tena. Ahadi ni deni. Tanu siku hiyo baba hakunywangi. Jumapili alienda kwa ibada na akaokoka. Watu walipoona amekoka walikuwa ne furaha kama tasa aliyepata mapacha. Mimi nikioa ningetaka kuwa mtu mtiifu kwa bibi yangi. Singetaka kunywa pombe, sigara au madawa ya kullevya. Ningetaku kuwa mtu wa kanisa. Kwenda kanisa ni lazima kamo ibada.

(Alama iliyotuzwa 23)

Mwandishi wa insha hii amelewa mada vizuri na amejaribu kuifuata katika kuandika insha yake. Ametumia lugha nzuri ya tamathali, lakini amefanya makosa mengi ya kisarufi na tahajia, kwa mfano:-

- |               |   |            |
|---------------|---|------------|
| • Hungenjua   | - | Hungejua   |
| • Gumbi gumbi | - | gubi gubi  |
| • Akajioga    | - | akaoga     |
| • Hakunywangi | - | hanywi nk. |